# K.C.P.E SHARPENER

## DARASA LA NANE MUHULA WA TATU - 2014

## KISWAHILI: LUGHA

SOMA MAAGIZO YAFUATAYO

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

**Muda: Saa 1 Dak. 40.**

I) JINA LAKO    II) JINA LA SHULE YAKO    III) NAMBARI YA MTIHANI

**Chagua neno mwafaka kukamilisha mtongo huu.**

Gari ni chombo cha manufaa sana kwetu. Sisi __1__ tunahitaji kuwa wenye __2__ kutokana na kuweko __3__ magari. __4__ kuna matwana ya aina __5__. __6__ hutumika kwa kusafirisha watu, bidhaa na shehena __7__ mizigo. Kuna matwana __8__ kibinafsi ambazo hubeba mtu na aila yake. Pia kuna matwana kwa kazi __9__.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | nyote | wote | sote | zote |
| 2. | himidi | joto | ghalabu | kiwewe |
| 3. | na | kwa | ya | la |
| 4. | ati | papo | kule | aidha |
| 5. | mingi | jingi | mengi | nyingi |
| 6. | malori | daladala | tingatinga | rukwama |
| 7. | la | cha | za | kwa |
| 8. | za | ya | la | wa |
| 9. | tele | kocho | chekwa | nyinginezo |

Sukari ni zao ambalo hutokana na __10__ wa mmea __11__ muwa. Wingi wake ni miwa. Hasa hupandwa __12__ kwa muda fulani kabla ya kuvunwa na kupelekwa __13__ ili majimaji yake matamu yakakamwe na kukaushwa ili kutengenzwa __14__. Bidhaa hii ni __15__ muhimu sana katika kinywaji cha chai.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 10. | upandaji | uchimbaji | upanzi | upandi |
| 11. | uitwayo | uitwao | itwayo | iitwao |
| 12. | mgundani | nyumbani | kiamboni | manzilini |
| 13. | dukani | sokoni | karakarani | kiwandani |
| 14. | dawa | chumvi | sukari | chai |
| 15. | kiungo | chakula | mlo | sehemu |

***Kuanzia swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo yake.***

16. Ni pambo lipi ambalo halifai kati ya mengine?
    A. Vipuli
    B. Herini
    C. Mapete
    D. Kidani

17. Chagua wingi wa: Mtume aliitengeneza meza yangu kisha akarudi kwake.
    A. Mitume alizitengeneza meza zangu
    B. Mitume walizitengeneza meza zetu kisha wakarudi makwao
    C. Watume walizitengeneza meza zenu kisha wakarudi makwao
    D. Mitume walizitengeneza meza zetu kisha wakarudi makwake

18. Kamilisha methali: Funika kawa ________
A. mwanaharamu apite
B. chakula kipoe
C. Wali usimwagike
D. lisipate uchafu

19. 'Ki' imetumikaje katika sentensi.
Atakapoondoka nitakuwa nikipika.
A. Kama kielezi
B. Kuonyesha masharti
C. Kuonyesha wakati
D. Kuonyesha ngeli

20. Maneno yaliyo na maana sawa ni ________
A. visawe B. vitate
C. vitawe D. vitatamshi

21. Maneno yafuatayo hutumika wakati wa ______

*Alamsiki* - *Binuru*
*Lala unono* - *wewe pia*
*Buriani* - *Buriani dawa*
*Tuonane kesho* - *Inshallah*

A. Maamkizi B. Adabu
C. Heshima D. Maagano

22. Andika kinyume cha sentensi hii:
Mgeni alitamani chakula kitamu.
A. Mgeni hakutamani chakula kitamu.
B. Mwenyeji alitamaushwa na chakula kichungu.
C. Mgeni alitamauka na chakula kichungu.
D. Mwenyeji alitamauka na chakula kitamu.

23. Tambua nomino ya mwisho katika orodha ya majina yafuatayo kulingana na kamusi.
A. Zuzuwaa B. Zuzu
C. Zumbukuku D. Zuka

24. Kipande cha tatu katika ushairi huitwa ______
A. utao B. mloto
C. mwandamizi D. ukwapi

25. Malipo ya kumshika mtoto mchanga kwa mara ya kwanza ni ________
A. fola B. fichuo
C. karadha D. mukafaa

26. Chagua sentensi yenye kivumishi kiashiria.
A. Kitabu changu ni kizuri.
B. Kitabu chenyewe kinavutia.
C. Kitabu hiki kilinunuliwa na baba.
D. Kitabu cha kwanza ni changu.

27. Ni sayari ipi ambayo ni ya pili kwa udogo na huchukua muda mrefu zaidi ya zote kuzunguka jua?
A. Zohali B. Utaridi C. Zuhura D. Dunia

28. Ni sentensi ipi sahihi?
A. Mocho aliandaa mankuli chapwa.
B. Mocho aliandaa mamkuli chapwa.
C. Mocho alihandaa mankuli chapwa.
D. Mocho aliandaa maakuli chapwa.

29. Jibu sahihi kwa maamkizi, "Habari?" ni ______
A. mzuri B. vyema
C. njema D. sijambo

30. Asilimia nukta ishirini na tano ni ________
A. 25.0% B. 2.5%
C. 250% D. 0.25%

***<u>Soma tukio hili kisha ujibu maswali 31 - 40.</u>***

Sossion ameupitisha usiku katika kupiga miayo kwingi na kuhesabu mitambaapanya, dalili wazi kwamba njaa ilikuwa ikiimuuma barabara. Katika hali hii hakuambulia hata lepe moja la usingizi. Kazi yake ya kusomba mizigo ya wasafiri kutoka kwenye vituo vya garimoshi na stani za matwana hadi katikati ya mji sasa imetumbukia nyongo. Kwani ametokea bepari fulani akaimwaga mikokoteni inayoitwa ipo siku, zaidi ya elfu sita inayowahudumia wasafiri kila mtaa.

Basi kulipokucha aliona si muruwa kuendelea kujikalisha mjini na kupakata mikono kama jeta. Aliazimia kuuhama mji arudi zake shambani huko kijijini Ahero, maana hakuona faida za mji. Rau kama angekata shauri kuendelea na ukaaji wa mji, basi ingemlazimu na kumjuzu kutafuta kibarua kingine. Nacho ni kipi ilhali yeye si msomi?

Mjini si maskani ya wazembe, la sivyo utakuwa kimelea au kupe mnyonyaji. Nao ukupe haukupi bila kuuma meno, labda uurefushe mkono au ukajiuze vichochoroni. Navyo vyote hivyo ni balaa kama si beluwa. Au tuviite starehe za mbwa kuukalia mkia kama si starehe za paka kunawia mate. Usiwe mtumwa wa njozi. Maisha si lelemama. Hakuna cha msalie mtume wala nabii. Kazi ni kujikaza.

31. Kwa nini Sossion hakupata usingizi?
A. Alipiga moyo konde
B. Alikuwa na njaa
C. Usingizi ulimpaa akipiga miayo
D. Hakuwa na kazi wala bazi

32. Sossion alikuwa na dhiki gani moyoni iliyomkera na kumkereketa?
A. Alifilisika
B. Alikosa usingizi usiku kucha
C. Alipiga miayo sana
D. Kibarua kilimwisha akawamba

33. Bila shaka, kwa mujibu wa habari hii, Sossion alikuwa ________
A. mhazili
B. mmachinga
C. hamali
D. mamanitilie

34. Kilichomvurugia Sossion mchuzi wake na kitumbua chake kuingia mchanga ni ________
A. wasafiri walipungua
B. alifukuzwa vituoni na kwenye stani
C. hakujua kuitumia mikokoteni ya "Ipo Siku"
D. idadi kubwa ya mikokoteni

35. Kinyume cha bepari ni ________
A. mkulima
B. kuli
C. kabaila
D. kabwela

36. Msemo "kujikalisha na kupakata mikono" si sawa na ________
A. kuwa mkunguni
B. kujikakamua
C. kuzembea
D. kuwa kupe

37. Kauli "uurefushe mkono" katika habari hii humaanisha nini?
A. Kufanya kazi kwa bidii
B. Kuwa mwizi
C. Kutafuta kibarua kingine.
D. Kujiuza vichochoroni

38. Aya ya mwisho inatushauri na kutunasihi kuwa
A. mjini ni makao ya wazembe
B. starehe za mjini ni za paka na mbwa
C. mtu hakai mjini bila msalie mtume au nabii
D. maisha ya mjini huhitaji watu wanaotafuta

39. "Nacho ni <u>kipi</u> <u>ilhali</u> yeye si <u>msomi</u>?" Maneno haya yaliyopigiwa msitari huitwaje kisarufi?
A. Kihusishi, kiunganishi, kivumishi
B. Kiulizi, kihusishi, nomino
C. Kivumishi, kilinganishi, mtenzi
D. Kiulizi, kiunganishi, nomino

40. Taarifa hii inatufunza kwamba ________
A. atafutaye hachoki, akichoka keshapata
B. mtegemea nundu haachi kunona
C. mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda
D. mchumia juani huvulia kivulini

***<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.</u>***

Mtihani! Ewe jinamizi usiyekuwa na huruma wala imani. Usiyejua mateso wala dhiki unayotupa. Usiku kucha tunakufikiria na mchana kutwa tunakushughulikia wewe.

Sisi, mwaka nenda mwaka rudi unatukeshesha na dhiki ni hizo hizo. Masomo yote tunayoyasoma unatuharibia maisha yetu katika muda wa saa chache ya mtihani. Eti tumeanguka! Mbona kusoma maswali tumeweza kuyasoma, si tungeanguka hapo! Mkono kuteleza kidogo ndio tumeanguka! Tumeanguka sisi au walimu! Mbona mpirani timu ikishindwa hawaambiwi wachezaji wameanguka au wameshindwa bali kocha ndiye anayefutwa kazi kwa kuwa yeye ndiye aliyeshindwa. Hakufanya matayarisho kabambe. Meneja ni sawa na wazazi, kwa hivyo katika mtihani, walaumiwe wazazi wala sio wanafunzi.

Ukweli ni kwamba unataka kutututa maana hakuna nafasi za kutoshea sote katika shule za upili ili tulemewe mapema. Aidha hamna pesa za kutulipia walimu wa shule hizo za upili lau zingekuwepo. Kwa hivyo, kizingizio ni kuanguka. Kwani wanaoanguka ndio wanaotupwa! Na lau sote twapita, mngetupeleka wapi?

Wangapi wanaokosana na wazazi wao kwa hiyo anguka yako? Wangapi wanafukuzwa kwa hiyo kuanguka! Ni wangapi wanaokatiza masomo na kuoa au kuoleka sababu ukiwa wewe? Je, ni wangapi wanaojiua kwa ukatili wako wa kuwaangusha! Yote haya ni kwa kuwa hujazaa kwani uchungu wa mwana ajua mama.

---

41. Anayesimulia makala haya ni ________
    A. mtahini
    B. mkurufunzi
    C. mtahiniwa
    D. mtihani
42. 'Mchana kutwa tunakushugulikia wewe,' kwa njia gani anashughulikiwa?
    A. Kudurusu, kusoma na kujibu mitihani siku zote
    B. Kutafuta karo, kutumwa nyumbani na kushiriki michezo
    C. Kusoma na kutalii
    D. Kwenda kazini, kupata mshahara na kupumzisha mwili
43. Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?
    A. Msimulizi ananasihi wanafunzi
    B. Msimulizi analaumu mitihani
    C. Msimulizi anasifu mitihani
    D. Msimulizi alifeli mtihani wake
44. Ni sababu gani, kwa mujibu wa msimulizi, haimo katika maelzo yake?
    A. Kuwapunguza wanafunzi
    B. Kukosekana walimu tosha katika shule za upili
    C. Wazazi kutoweza karo ya shule za upili
    D. Upungufu wa shule za upili
45. Katika ibara ya mwisho, kuna maafa mangapi ya kuanguka mtihani?
    A. 4 B. 3
    C. 2 D. 5
46. Kufuatana na msimulizi, ni nani alaumiwe?
    A. Kocha
    B. Wanafunzi
    C. Meneja
    D. Wazazi
47. Badala ya 'dhiki ni hizo hizo' lingetiliwaje mkazo?
    A. hizo zote
    B. hizo zimu
    C. zizo hizo
    D. mumo
48. Mwandishi anaweza kujibiwa na methali isemayo ________
    A. Usipoziba ufa, utajenga ukuta
    B. Asiyesikia la mkuu huvunjika mguu
    C. Bidii ya mja haiondoi kudura
    D. Usishindwe na mapishi ukasingizia moshi
49. Maana ya kutututa ni ________
    A. kutopita mtihani
    B. kubebeshwa majukumu tusiyoweza
    C. kufeli mtihani
    D. kupunguza idadi
50. Kichwa mwafaka ni ________
    A. Wanafunzi wanafeli
    B. Mtihani
    C. Majukumu ya watahini
    D. Mitihani ni migumu